

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA NNE

28 APRILI, 2017



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA NNE – TAREHE 28 APRILI, 2017

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

110. **MHESHIMIWA ESTHER MICHAEL MMASI**
(VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Pamoja na juhudi za Serikali katika kulinda ajira za vijana wa Kitanzania Serikali kupitia Sheria ya Ajira ya Wageni Na.1 ya Mwaka 2015 ilirasimisha vibali vya kuishi na ajira kwa wageni batili wapatao 317 kati ya 779:-

Je, ni vigezo gani vilivyotumika katika urasimishaji wa vibali hivyo wakati vijana wengi wa Kitanzania hususan wahitimu wa Vyuo Vikuu wanahangaika katika kupata ajira ili wafurahie faida ya taaluma zao.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

111. MHESHIMIWA VENANCE METHUSALAH MWAMOTO (KILOLO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Vyanzo vingi vya maji vinavyojaza Bwawa la Kihansi vinatoka Wilaya ya Kilolo:-

Je, Wilaya hii inanufaika vipi.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

112. MHESHIMIWA VICTOR KILASILE MWAMBALASWA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye Kata za Ifumbo, Lualaje, Mafyeko na Kambikatoto katika Wilaya ya Chunya.

113. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Mkoa wa Kigoma una madini ya Chokaa, Dhahabu, Platinum n.k.:-

Je, Serikali imechukua hatua gani kuendeleza utafutaji na uchimbaji wa madini katika Mkoa huo.

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

114. MHESHIMIWA GODBLESS JONATHAN LEMA (ARUSHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Agizo la Mhe. Rais la kufufua viwanda ni muhimu na la msingi kwa maendeleo ya Taifa.:-

Je, Serikali haioni mradi wa Kurasini Logistic Center unakwenda kinyume na fikra za Mhe. Rais kuhusu viwanda.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

115. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLAH SALIM (MTAMBILE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Serikali imesema ina mkakati wa kujenga viwanda katika Mkoa wa Mtwara, lakini njia ya usafirishaji wa mizigo inayotumika ni barabara tu, hali inayosababisha barabara hiyo kuwa na uwezekano wa kuharibika kwa haraka:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha Meli ya Mizigo itakayotoka Dar es Salaam kwenda Mtwara ili kuinusuru barabara hiyo isiharibike.

116. MHESHIMIWA OMAR ABDALLAH KIGODA (HANDENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je ni lini Kampuni ya Simu iliyofunga mnara wake katika Kijiji cha Kwamatutu itauwasha ili Wananchi wapate huduma.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

117. MHESHIMIWA FELISTER ALOYCE BURA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Serikali imeanzisha Benki ya Kilimo kwa lengo la kusaidia Wakulima wakubwa na wadogo kupata mikopo ya pembejeo kwa haraka:-

Je, ni lini Benki hiyo itanza kutoa huduma kwa Wakulima wadogo wadogo wa Mkoa wa Dodoma.

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

118. MHESHIMIWA SIXTUS RAPHAEL MAPUNDA (MBINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Moja kati ya changamoto zinazowakabili Wakulima wa Kahawa ni kodi na makato mengi:-

Je, ni lini Serikali itazipiga marufuku kodi zote zinazomnyonya Mkulima.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
28 APRILI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**